

AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA



UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax:
+251 115 517 844
Website: www.au.int

Kumbukumbu: BC/OLC/66.5/18532.26

Kamisheni ya Umoja wa Afrika inatoa pongezi zake za dhati kwa Misheni za Kudumu za Nchi zote Wanachama katika Umoja wa Afrika, na ina heshima ya kurejelea suala la uanachama wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (AfCHPR).

Kamisheni inapenda kuzitaarifu Misheni za Kudumu kwamba muda wa utumishi wa Majaji wafuatao wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (AfCHPR) utaisha mwezi Februari 2027:

NA.	JINA	NCHI	MUDA WA UTUMISHI
1.	Bi. Iman D. ABOUD	Tanzania	Alichaguliwa tena mwezi Februari 2021 kwa kipindi cha miaka sita
2.	Bw. Rafaa BEN ACHOUR	Tunisia	Alichaguliwa tena mwezi Februari 2021 kwa kipindi cha miaka sita
3.	Bw. Dumisa Buhle NTSEBEZA*	Afrika Kusini	Alichaguliwa mwezi Februari 2021 kwa kipindi cha miaka sita
4.	Bw. Modibo SACKO*	Mali	Alichaguliwa mwezi Februari 2021 kwa kipindi cha miaka sita

** Majaji waliotajwa katika namba 3 na 4 wanastahili kuchaguliwa tena.*

Kwa hiyo, Kamisheni inapenda kuzitaarifu Misheni za Kudumu kwamba uchaguzi na uteuzi wa **Majaji wapya wanne (4)** utafanyika wakati wa Mkutano wa Kawaida wa 50 wa Baraza Kuu, uliopangwa kufanyika Januari 2027.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, Kamisheni inazialika **NCHI ZILIZORIDHIA** Itifaki ya Mkataba wa Afrika ya Haki za Binadamu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Itifaki) ambazo zinakidhi vigezo, kuwasilisha mapendekezo ya wagombea/uteuzi wa wagombea, yakiambatanishwa na wasifu wa wagombea (CV), kwa njia mojawapo kati ya zifuatazo: katika **BAHASHA ILIYOFUNGWA NA KUGONGWA MHURI, INAYOWASILISHWA KWA OFISI YA MSHAURI WA SHERIA, KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA**, au kuwasilishwa katika Ofisi ya Usajili ya Mshauri wa Sheria kupitia anwani ya

baruapepe ifuatayo: OLC-Elections@africanunion.org, nakala kwa Fikerteb@africanunion.org **TAREHE AU KABLA YA TAREHE 30 NOVEMBA 2026.**

Wasifu wa Kitaaluma (CV) unapaswa kuandikwa kwa kuacha nafasi moja ya msitari, usizidi kurasa tatu (3), na uwasilishwe katika angalau lugha mbili (2) za kazi za Umoja wa Afrika. Muundo wa wasifu huo umeambatishwa hapa kwa ajili ya kurahisisha urejeleaji. Aidha, CV inapaswa kuwasilishwa katika nakala laini (muundo wa Word).

Kwa muktadha huu, Kamisheni inapenda pia kuzitaarifu Misheni za Kudumu kuhusu masharti mahususi ya Itifaki yafuatayo:

Ibara ya 11 ya Itifaki kuhusu Muundo wa Mahakama:

- “1. Mahakama itakuwa na Majaji kumi na moja (11), ambao ni raia wa Nchi Wanachama wa OAU (AU), watakoachaguliwa kwa nafasi zao binafsi miongoni mwa wanasheria wenye maadili ya kiwango cha juu na wenye umahiri na uzoefu unaotambulika katika utekelezaji wa sheria, shughuli za kimahakama au umahiri wa kitaaluma katika nyanja ya haki za binadamu na haki za watu.
2. Hakutakuwa na Majaji wawili wenye uraia wa Nchi moja.”

Ibara ya 12 itifaki kuhusu Uteuzi wa Wagombea:

- “1. Nchi Wanachama wa Itifaki zinaweza kila moja kupendekeza hadi wagombea watatu (3), ambapo angalau wawili (2) kati yao wanapaswa kuwa raia wa nchi hiyo.
2. Uwakilishi wa kijinsia unapaswa kuzingatiwa katika mchakato wa uteuzi wa wagombea.

Ibara ya 14 Itifaki kuhusu Uchaguzi:

....

- “2. Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali utahakikisha kuwa Mahakama kwa ujumla inawakilisha kanda kuu za Afrika na mifumo yake mikuu ya kisheria.
3. Katika uchaguzi wa Majaji, Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali utahakikisha kuwa kuna uwakilishi wa kutosha wa kijinsia.”

Hivyo, Nchi Wanachama zinaweza kuteua raia wao wenyewe kuwa wagombea, kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa katika Ibara ya 12. Hata hivyo, wagombea hawawezi kuteuliwa kutoka Nchi Wanachama ambazo tayari zina Majaji katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, ambazo ni **Aljeria, Kameruni, Jamhuri ya Kongo, Ghana, Malawi, Nigeria na Uganda.**

Aidha, pale ambapo Nchi Mwanachama wa Itifaki itamteua mgombea ambaye si raia wake, mgombea huyo lazima awe raia wa Nchi Mwanachama ambayo haijawekewa vikwazo vya kiwango cha kati au vikwazo vya Juu. Hili linaendana na Kanuni ya 36 ya Kanuni za Uendeshaji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, ambayo inazuia Nchi Wanachama zilizowekewa vikwazo hivyo kuteua raia wake katika nafasi zinazojazwa kwa uchaguzi au nafasi nyingine zisizojazwa kwa uchaguzi.

Nchi Wanachama wa Itifaki zinakumbushwa tena kuzingatia ipasavyo uwakilishi wa kutosha wa kijinsia katika mapendekezo yao ya wagombea, na kuzingatia masharti yaliyotajwa hapo juu, pamoja na Uamuzi EX.CL/907 (XXVIII) Rev.1 kuhusu Taratibu za Utekelezaji wa Vigezo vya Uwakilishi wa Haki wa Kijiografia na Kijinsia katika Vyombo na Taasisi za Umoja wa Afrika, uliopitishwa na Baraza Kuu mwezi Januari 2016. Aya ya 2 ya Uamuzi huo inasema kama ifuatavyo:

- “i) Uwakilishi wa kikanda, pale inapofaa, utakuwa kama ifuatavyo: Afrika Mashariki (2), Afrika ya Kati (2), Afrika Kaskazini (2), Afrika Kusini (2) na Afrika Magharibi (2), isipokuwa katika hali ambapo Kanda imejulishwa rasmi na halijawasilisha wagombea;*
- ii) Pale inapohitajika, nafasi moja (1) itakuwa nafasi ya mzunguko kati ya kanda tano (5) za Afrika;*
- iii) Angalau mjumbe mmoja (1) kutoka kila kanda ya Afrika lazima awe mwanamke;*
- iv) Taratibu hizi zitaanza kutumika mara moja.*

Kwa kuzingatia maelezo yaliyotangulia, Kamisheni inapenda kuzitaarifu Misheni za Kudumu kwamba uwakilishi wa kikanda na kijinsia katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (AfCHPR), baada ya kumalizika kwa muda wa utumishi wa Majaji wanne (4) waliotajwa hapo juu, utakuwa kama ifuatavyo:

a) Uwakilishi wa Kikanda

Kati	: Mbili (2)
Mashariki	: Moja (1)
Kaskazini	: Moja (1)
Kusini	: Moja (1)
Magharibi	: Mbili (2) [Mmoja (1) akichukua nafasi ya mzunguko]¹

b) Uwakilishi wa Kijinsia

Majaji Wanawake	: Wanne (4)
Majaji Wanaume	: Watatu (3)

¹ Nafasi ya mzunguko kati ya kanda tano za Afrika kwa sasa inashikiliwa na Jaji Dennis Dominic ADJEI (mwanaume, raia wa Ghana), aliyechaguliwa mwezi Julai 2022 kwa kipindi cha miaka sita.

Kwa kuzingatia maelezo yaliyotangulia, **Nchi Wanachama za Itifaki zinazokidhi vigezo** ² **kutoka katika Kanda za Afrika Mashariki, Kaskazini, Kusini na Magharibi** zinaombwa kuwasilisha mapendekezo ya wagombea/uteuzi wa wagombea kwa Ofisi ya Mshauri wa Sheria, kwa kuzingatia masharti na tarehe ya mwisho iliyotajwa hapo juu, kama ifuatavyo:

- **Kanda ya Mashariki:** Mmoja (1) mgombea mwanamke
- **Kanda ya Kaskazini:** Mmoja (1) mgombea mwanaume
- **Kanda ya Kusini:** Mmoja (1) mgombea mwanaume
- **Kanda ya Magharibi:** Mmoja (1) mgombea mwanaume

Pia, Kamisheni inasisitiza kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 11(1) ya Itifaki, wagombea waliopendekezwa wanapaswa kuwa na **“...maadili ya kiwango cha juu na umahiri pamoja na uzoefu unaotambulika katika utekelezaji wa kisheria, shughuli za kimahakama au umahiri wa kitaaluma katika nyanja ya haki za binadamu na haki za watu.”**

Wagombea wanapaswa pia kuwa na uzoefu katika angalau mojawapo ya mifumo mikuu ya kisheria ya Afrika, ikiwamo mfumo wa sheria za kiraia, mfumo wa sheria za kawaida, sheria za Kiislamu na sheria za kimila za Kiafrika.

Aidha, Kamisheni inapenda kutoa msisitizo kwa Misheni za Kudumu kuhusu Ibara ya 18 ya Itifaki inayohusu Kitoingiliana na wadhifa (Incompatibility), ambayo inaeleza kama ifuatavyo:

“Wadhifa wa Jaji wa Mahakama hauwezi kuingiliana na shughuli yoyote inayoweza kuathiri uhuru au kupendelea upande wowote kwa Jaji huyo, au mahitaji ya wadhifa huo, kama yatakavyoainishwa katika Kanuni za Utaribu za Mahakama.”

Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Mahakama inaeleza zaidi kwamba:

“Majaji hawaruhusiwi, hususan, kushikilia nyadhifa za kisiasa, kidiplomasia au kiutawala, wala kufanya kazi kama washauri wa kisheria wa Serikali.”

Kwa kutoa mwongozo kuhusu kuingiliana kwa wadhifa na shughuli nyingine, Kamati ya Ushauri ya Wanasheria kuhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Kudumu ya Haki ya Kimataifa (PCIJ), ambayo kwa sasa ni Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ), ilieleza kwamba:³

“[A] Mwanachama wa Serikali, Waziri au Naibu Katibu wa Nchi, mwakilishi wa kidiplomasia, mkurugenzi wa wizara au walio chini yake, au mshauri wa kisheria wa wizara inayoshughulikia mambo ya nje, ingawa wanaweza kustahili kuteuliwa kuwa wasuluhishi katika Mahakama ya Kudumu ya Usuluhishi ya mwaka 1899, kwa hakika hawastahili kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama yetu.”

² Isiyowekewa vikwazo kutokana na mabadiliko ya Serikali yasiyozingatia Katiba, au vikwazo vya kiwango cha kati au cha juu

³ Tazama PCIJ/Advisory Committee of Jurists. *Procès-Verbaux of the Proceedings of the Committee. June 16-July 24 1920*, 693, 715-716 (1920)

Kwa hiyo, Nchi Wanachama zinazokidhi vigezo zinaombwa kuhakikisha kuwa wagombea wanaowapendekeza wanawasilisha taarifa za kina za wasifu wao, zikieleza uzoefu wao katika shughuli za kimahakama, utendaji wa kisheria, umahiri wa kitaaluma, kazi za kitaaluma na uzoefu mwingine wowote unaohusika katika nyanja ya haki za binadamu na haki za watu. Taarifa hizo zinapaswa pia kubainisha uhusiano wa kisiasa na uhusiano mwingine unaohusika katika kutathmini kustahiki kwa wagombea na uwezekano wowote wa kutoingiliana kwa wadhifa wa Jaji na shughuli nyingine. Aidha, wagombea wanapaswa kuwasilisha maelezo yanayoeleza jinsi wanavyokidhi vigezo vya kustahiki vilivyowekwa katika Itifaki.

Misheni za Kudumu zinapaswa kuzingatia kwamba Kamisheni haitaweza kushughulikia nyaraka au maombi yoyote ambayo hayatazingatia masharti ya lazima yaliyobainishwa hapo juu.

Mbali na masharti ya lazima yaliyotajwa hapo juu, Nchi Wanachama zinaweza pia kuzingatia mapendekezo yafuatayo yaliyowasilishwa kwa Kamisheni na asasi za kiraia:

- a) Utaratibu wa kuteua wagombea unapaswa kukidhi, angalau, viwango vinavyotumika katika uteuzi wa kushika wadhifa wa juu zaidi wa kimahakama katika Nchi Mwanachama husika;
- b) Nchi Wanachama zinapaswa kuhamasisha ushiriki wa vyombo vya mahakama na vyombo vingine vya Serikali, vyama vya wanasheria, taasisi za kitaaluma na za haki za binadamu, makundi ya wanawake, pamoja na mashirika mengine ya asasi za kiraia katika mchakato wa kuwachagua wagombea watakaopendekezwa; na
- c) Nchi Wanachama zinapaswa kutumia utaratibu wa kitaifa wa kuwachagua wagombea ulio wazi na usiopendelea upande wowote, ili kuimarisha imani ya umma katika uadilifu wa mchakato wa uteuzi wa wagombea.

Kamisheni ya Umoja wa Afrika inatumia fursa hii kuzihakikishia upya Misheni za Kudumu za Nchi zote Wanachama heshima yake ya dhati na ya hali ya juu.



Addis Ababa, 16 Oktoba 2026

H.G.

Kwa: Misheni za Kudumu za Nchi zote Wanachama katika Umoja wa Afrika
Addis Ababa

MUUNDO WA MAOMBI YA KAZI WA UMOJA WA AFRIKA

NAFASI:

1. TAARIFA BINAFSI

1.1 JINA

1.2 ANWANI YA MAWASILIANO

1.3 ANWANI YA MAKAZI

1.4 BARUAPEPE

1.5 JINSIA

1.6 UTAIFA

1.7 TAREHE YA KUZALIWA (SIKU/MWEZI/MWAKA)

2. SIFA ZA KIELIMU

3. MUHTASARI WA UJUZI NA UTAALAMU WA KIKAZI

4. MUHTASARI WA UZOEFU WA KAZI UNAOHUSIANA NA NAFASI INAYOOMBWA

5. ORODHA YA MACHAPISHO (KAMA YAPO)

6. UJUZI WA LUGHA (KIARABU, KIINGEREZA, KIFARANSI, KIRENO, KIHISPANIOLA, KISWAHILI)

7. TAARIFA NYINGINE MUHIMU NA ZA KUUNGA MKONO MAOMBI

8. SHUGHULI ZA BURUDANI UNAZOPENDA

9. WADHAMINI (WASIOPUNGUA 3)